

# Pambazuko

Toleo Namba 068

Jumatatu Aprili 8-14, 2024



Jicho la Tai

Samia aksante,  
ila kwa Makonda  
shida!

UK. 5

UK. 11-13

## Tanzania yageuka pango la 'kubeti'

● *Ni tishio jipya afya ya akili*

Ruto abadili gia, upinzani wamkubali-UK. 14

**BoT yaongeza  
riba. Je, wajua  
athari?**

UK. 6

**Rostam kutumia  
bil. 29/- kunakshi  
Mwanza**

UK. 7

**John Heche  
'amvaa'  
Shabiby**

UK. 8



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye  
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Tahariri

## Refa huyu kaharibu. Ni adui wa mpira

**W**APENZI wa mchezo unaopendwa zaidi duniani, mpira wa miguu, au ukiitwa soka na Tanzania ukijulikana zaidi kwa jina la kabumbu, watakuwa wamekerwa mno na uamuzi wa kuwanyima goli la wazi, timu ya Yanga kutoka Tanzania.

Yanga ilidhulumiwa goli lililoingizwa kimiani mwanzoni mwa kipindi cha pili na mchezaji wake, Aziz Ki, katika dakika ya 58, baada ya kupiga shuti ambalo liligonga mwamba na kutumbukia ndani ya goli la wapinzani wao, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Mchezo huo wa robo fainali ya Kombe la Klabu Bingwa Afrika, ulichezwa katika dimba la Loftus Versfeld, jijini Pretoria Afrika Kusini juzi – Ijumaa, Aprili 5, 2024.

Katika mchezo huo, mwamuzi (refa) kutoka Mauritania, Dahane Beida, alipuliza kipyenga kumaliza mchezo huo ndani ya dakika 95, timu zote zikiwa hazijafungana.

Hata hivyo, kulingana na kanuni za mchezo huo, timu zililazimika kwenda kwenye mikwaji ya penati ili kumpata mshindi, ambapo Yanga iliyaaga mashindano hayo kwa kufungwa mabao 3:2.

Uamuzi wa Dahane Beida kuwanyima Yanga goli la wazi, umelaaniwa na wapenzi wa soka, huku wengi wakieleza kuwa huenda mchezo huo ulikuwa umepangwa na “wakubwa” kwamba Yanga ya Tanzania lazima iage mashindano hayo.

Mitandao ya kijamii, kutoka maeneo mbalimbali ya dunia, wamelaani mwamuzi huyo na kueleza kuwa huenda alikuwa na “maelekezo ya

kuhakikisha Yanga haisongi mbele.”

Katika mazingira yoyote, nasi gazeti la Pambazuko tunaungana na wapenzi wa mpira wenye mtazamo kwamba mwamuzi wa mchezo huenda alikuwa na maelekezo yenye kubeba ushawishi ambao sisi hatuuji.

Pambazuko tunajiuliza, iweje mwamuzi huyo akaamua kukataa goli la wazi namna ile ambalo, hata wasiokuwa wafuatiliaji wa mpira wa miguu na wasiojua sheria za soka, wamebaini pasina shaka, kwamba mpira uliingia kimiani.

Hatuamini kwamba mwamuzi anayevaa beji ya Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), hajui sheria za mchezo huo, isipokuwa huenda kuna kitu kilivuruga “ubongo” wake hata kuonekana mjinga wa sheria anazosimamia.

Uamuzi huo wa hovyoyote, umeichafua Afrika na hasa taasisi zinazosimamia mchezo huo, ikiwamo Shirikisho la Soka Afrika (CAF), huku wengi wakieleza kuwa bara hilo haliwezi kuendelea iwapo litakumbatia rushwa na hata kupanga matokeo.

Yanga kunyimwa halali yake, kumemfanya hata kocha wa Mamelodi, Rhulani Mokwena kukataa kuzungumza lolote kuhusu goli hilo, huku akisisitiza kuwa “Yanga ni timu ngumu na wamecheza kufa na kupona. Tunawahesimu.”

Pambazuko tunasema mwamuzi huyo ni mjinga wa sheria anazozitambua na hatuoni haya kumlaani na kuomba vyama vya soka vya kimataifa kuchukua hatua dhidi ya mwamuzi huyo kwa kuwa ameonyesha ujinga na kutukanisha soka la Afrika.

## TMDA KIDEDEA...



*Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi, akimkabidhi tuzo Gaudensia Simwanza, Meneja Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) baada ya kuibuka mamlaka hiyo kuibuka washindi wa taasisi yenye uhusiano imara na vyombo vya habari. Tuzo hizo hutolewa na Chama cha Maofisa Mawasiliano Tanzania (PRST). Hafla hiyo ilifanyika Dar es Salaam, April 5, 2024. (Picha na Mpigapicha Wetu).*

### Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

**NUKUU**



*“Mipango mingi ya serikali yetu (Tanzania), inashindwa kuendelea wala kuleta matokeo chanya na makubwa, kwa kuwa kila baada ya muda mfupi, inabadilika ama kuachwa kabisa kwa kuwa kila kiongozi, anayeingia madarakani, anakuwa na matamano yake – Mchungaji Peter Msigwa.*

## Tangazo

## Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,**  
**Oktoba, 2023**

## Changia Pambazuko liendelee

**WAJUMBE** wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

**Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263**

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandaa: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



## **Samia aksante, ila kwa Makonda shida!**

Na Igo AI

**L**EO Mzee Tai kaamka kwa bashasha; Huso wake unaonekana umebeba furaha inayothibitishwa na sauti ya unyenyekevu inayosikika alipomuita kijana wake wa kazi.

Katoka chumbani kwake akiwa kavalia tisheti ya njano yenye picha ya Rais Samia Suluhu Hassan iliyoandikwa – “Mitano Tena.”

Hajavaa msuli kama kawaida yake, ila kajifunga taulo jeupe, ambalo kwa karibu linaonekana kufubaa maana limekuwa la muda mrefu. Analipenda kwelikweli taulo hilo eti akidai alinunua Marekani!

“Haya leo tunapata brekifasti gani, kuna kuku frijini? Tengeneza mchemsho na agiza chapati,” hii ilikuwa kauli ya mwanzo ya Mzee Tai baada ya kupokea salamu kutoka kwa kijana wake wa kazi.

Kijana wa Mzee Tai akaeleza kwamba friji haina kitu! Basi, mwenye nyumba akaingia chumbani kwake na baadaye akatoka akiwa na noti kadhaa za elfu kumu-kumi.

“Nenda kanunue kuku wawili - wa kienyeji, chukua mvinyo wangu, leta sharubati na mazagazaga mengine, harakisha maana nimemka nina njaa kali,” aliagiza Mzee Tai.

Je, furaha ya Mzee Tai leo imetoka wapi?

Kumbe Mzee Tai kajawa furaha baada ya ushauri wake kwa Rais Samia Suluhu Hassan kufanyiwa kazi kwani wiki iliyopita, alimshauri kiongozi huyo wa nchi kumpangia kazi nyingine, Fakiu Lulandala, ambaye hadi ‘majuzi’ alikuwa Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM).

Kutokana na ushauri wa Mzee Tai, Rais Samia alimpangia kazi nyingine Lulandala. Sasa anakuwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, huko Mkoa wa Manyara.



*Paul Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Arusha*

Ushauri wa Mzee Tai kumuasa Rais Samia ampangie majukumu mengine Lulandala, ulitokana na kauli yake kwamba – “ukosefu wa ajira kwa vijana Tanzania ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na CCM.”

Lulandala alidai kwamba kuboreshwa kwa mazingira mazuri ya elimu nchini, kumefanya vijana wengi kupata uwezo wa kufanya kazi, lakini kwa kuwa ajira ni finyu, na wao ni wengi, ndiyo maana wanakuwa “mitaani wakizurura.”

Kauli hii ilimchefua Mzee Tai na kuamini kwamba “anakichafua” chama chao, hivyo kumpa ushauri mwenyekiti wa CCM, Rais Samia, ambaye bila kinyongo, kamsikia na kutekeleza.

Hata hivyo, pamoja na furaha ya Mzee Tai, wakati akiwa mezani “akikamata” supu ya kuku, akasema Rais Samia amekosea kumpa Paul Makonda dhamana ya kuongoza Mkoa wa Arusha, kwani anadhani kiongozi huyo atatumia muda mrefu zaidi kupambana na wapinzani, hasa Godbless Lema, huku akisahau kupigania maendeleo ya umma mpana.

Kwamba kwa ubabe wa Makonda, Mzee Tai anadhani nguvu nyingi ataweka kujenga chama chake na kusahau kilichompeleka, kwani damu yake imekolea kijani na njano zaidi.

## Habari

**BoT yaongeza riba. Je, wajua athari?**

Na Mwandishi WETU

**B**ENKI Kuu ya Tanzania imepandisha riba ya mikopo yake kutoka asilimia 5.5 iliyotumika katika robo ya kwanza ya mwaka huu hadi asilimia 6.

Riba hiyo mpya itatumika katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka huu. Robo hiyo inaanza Aprili hadi Agosti, 2024.

BoT imeliambia Pambazuko kwamba uamuzi huo umezingatia tathmini ya mwelekeo wa hali ya uchumi nchini Tanzania iliyofanyika Machi, mwaka huu.

Wataalamu wa masuala ya uchumi na fedha waliozungumza na Pambazuko wameeleza kuwa hatua hiyo itakuwa na manufaa, lakini pia athari hasi katika mambo kadhaa kwenye uchumi ikiwemo gharama za mikopo, matumizi, uwekezaji na thamani ya shilingi kwa kutaja mambo machache.

BoT, imeeleza kuwa utekelezaji wa sera ya fedha katika robo ya kwanza ya mwaka huu ulifanya riba ya mikopo ya siku saba katika soko la jumla la fedha baina ya benki, kubaki ndani ya wigo asilimia 3.5 hadi asilimia 7.5 kama ilivyotarajiwa.

“Utekelezaji wa sera ya bajeti ulikuwa wa kuridhisha, ambapo katika robo ya kwanza ya mwaka 2024, mapato ya serikali yalikuwa takriban asilimia 95 ya lengo kwa Tanzania Bara,” imeeleza BoT.

Kwa upande wa Zanzibar, BoT imesema kuwa mapato ya ndani yalivuka lengo kwa asilimia 6.4 katika kipindi hicho.

Katika hilo, wataalamu wa uchumi wanaonya kuwa kuna uwezekano mkubwa wa mapato ya serikali kupungua katika robo ya pili kwa sababu ongezeko hilo la riba linaweza kusababisha kupungua kwa matumizi kutokana na kupungua kwa mikopo kunakosababishwa na kuongezeka kwa gharama za kukopa.

Wataalamu hao wanaeleza kuwa kwa kawaida, wakati ambapo Benki Kuu inaongeza riba, gharama za kukopa zinakwenda juu kwa wafanyabiashara na wataja wengine wa kawaida.

Jambo hilo linaweza kusababisha



*Gavana BoT - Emmanuel Tutuba*

kushuka kwa mikopo, hivyo kupunguza kiwango cha matumizi kama vile ununuzi wa magari na ujenzi wa nyumba na hivyo kuyumbisha uchumi.

Aidha, imebainika kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka huu, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kwa asilimia 1.8 ikilinganishwa na asilimia 1.6 katika robo ya tatu ya mwaka 2023.

Pamoja na athari hasi, zipo chanya, ambapo wachumi wanabainisha kuwa riba kubwa zinaweza kuvutia zaidi uwekezaji kutoka nje na hivyo kuongeza mahitaji ya sarafu zinazotumika kuagiza bidhaa kutoka nje hasa dola ya Marekani.

Hilo litashusha thamani ya shilingi na kufanya gharama za kuagiza bidhaa nje ya nchi kupanda, huku thamani ya mauzo ya nje ikishuka.

Pamoja na kuathiri thamani ya shilingi pia hali hiyo itasababisha kupanda kwa urari wa biashara.

Wataalamu hao wa uchumi na fedha pia wameliambia Pambazuko kuwa riba kubwa zinaweza kuongeza kasi ya kuweka akiba na uwekezaji, kwani wafanyabiashara watavutika kuweka akiba kutokana na kuvutiwa na riba kubwa watakayopata.

Mchumi mbobezi katika masuala ya fedha, Dkt. Julius Kapwani anasema kuwa kawaida ongezeko la riba

## **Rostam kutumia bil. 29/- kunakshi Mwanza**

Na Mwandishi WETU

**J**IJI la Mwanza litaongezwa nakshi ya Jurembo, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kisasa la abiria katika uwanja wake wa ndege.

Kandarasi ya ujenzi wa jengo hilo litakalokuwa na uwezo wa kuchukua abiria 600 kwa wakati mmoja, iko mikononi mwa mfanyabiashara mzawa, Rostam Aziz kupitia kampuni yake ya Taifa Mining & Civils Limited.

Kampuni hiyo ambayo iko daraja la kwanza, ilitia saina mkataba wa ujenzi wa mradi huo Machi 29, 2024 na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA).

Kampuni ya Rostam imepewa miezi 10 kukamilisha kazi hiyo.

Taifa Mining imekuwa ikifanya kazi ya ukandarasi katika migodi na kwamba ina ujuzi wa zaidi ya 20 kwenye kada hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Mussa Mbura amesema kuwa kuwepo kwa jengo hilo la kisasa katika Jiji la Mwanza, kutaongeza nakshi na mvuto kwa wageni na wenyeji wanaotumia uwanja wa ndege wa jiji hilo.

Jengo la abiria lililoanza kujengwa awali, mwaka 2019, wakati wa uongozi wa Rais John Magufuli, lilisimama baadaye baada ya kubainika kuwa na kandarasi wasiokuwa na uwezo mkubwa



*Rostam Aziz*

wa ujenzi wa majengo ndani ya viunga vya viwanja vya ndege.

Ujenzi wa awali, ulisimamiwa na mamlaka za Mkoa wa Mwanza, baada ya kuamuriwa na serikali iliyopita, wakati wahusika wakiwa na ukomo wa ujuzi katika mchakato wa ujenzi wa aina hiyo.

## **BoT yaongeza riba. Je, wajua athari?**

*Inatoka Uk. 6*

linaweza kubadili tabia za watu, hasa wafanyabiashara kwa sababu badala ya kutumia fedha zao, sasa watataka kuziweka benki kwani zitapata riba kubwa na hii inaweza kupunguza mzunguko wa fedha kwenye soko.

Hata hivyo, msomi huyo anahadharisha kuwa ongezeko la riba linaweza kusababisha kushuka kwa uwekezaji wa ndani, kwani wawekezaji wengi watatishwa na gharama kubwa za

kupata mikopo kwa ajili ya uwekezaji, hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

Kuhusu athari za riba kubwa kwenye deni la taifa, mchumi huyo anasema kuwa mara nyingi serikali inakopa kutoka masoko ya fedha ya ndani na kuongezeka kwa riba nako kutaongeza gharama za mikopo hiyo na kutaongeza matumizi kwenye malipo ya madeni na kuathiri matumizi ya serikali kwenye miradi ya maendeleo.

## Habari

## Heche 'amvaa' Shabiby kwenye bima

Na Mwandishi WETU

**M**JUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), John Heche, amekiambia Chama cha Mapinduzi (CCM) kuacha mara moja kufikiria "kukamua" zaidi fedha za Watanzania.

Heche akizungumza na Pambazuko jana amesema ushauri wa Mbunge wa Gairo (CCM), Ahmed Shabiby kuwa serikali ikate shilingi 2,000 kila mwezi kwenye laini za simu ili fedha hizo zichangie mapato kwa bima ya afya kwa wote, "siyo sawa."

"Wananchi wetu ni masikini sana, halafu anaibuka mbunge, anayelipwa mamilioni ya fedha kila mwezi, kutaka serikali ikate fedha kwa watu masikini, hii haitakuwa sawa, itaongeza umasikini zaidi," amesema Heche.

Heche ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Tarime (Chadema) amesema Shabiby na chama chake, wasiwe na mawazo ya kuendelea "kuwaumiza wananchi" kwa kodi zingine kubwa, hiyo itawafanya kuwa na uchumi mbaya.

Ijumaa iliyopita – Aprili 5, Shabiby aliishauri serikali, wakati akichangia mapendekezo ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Shabiby alisema kuwa Tanzania ina wamiliki wa laini za simu milioni 72 ambao makato yao kwa mwaka yataingiza shilingi trilioni 1.72, ambazo zitaelekezwa mfuko wa bima ya afya kwa wote ili wananchi wapate matibabu bila kusuasua.

Tanzania ilipitisha sheria ya Bima ya Afya kwa Wote mwaka jana, lakini undeshaji wake bado haujawa wazi, hasa namna itakavyopata fedha za uhakika.

"Nimeona tulizungumzie bila woga, najua kuna mawazo tutatoa na watu watatukana kwenye mitandao, lakini acha watukane. Hii bima ya afya, ushauri



John Heche

ninaotoa tupende tusipende, lazima tuingize chanzo cha muhimu ambacho tutakipata kwa urahisi," alisema Shabiby.

Heche alisema serikali ina fedha nyingi "zinazopotea kwa matumizi ya hovyo," ambazo zingeweza kugharimia masuala ya bima kwa wote, bila kuangalia namna ya kuongeza mzigo wa kodi kwa watu masikini kupitia laini zao za simu.

"Watu wetu ni masikini, wangeachwa waendeleo kuishi, bila kuwapa mzigo mwingine wa ugumu wa maisha, hii serikali ya CCM, ina matumizi makubwa yasiyokuwa ya lazima, hizo fedha za anasa kwa viongozi, ndiyo zikalipe gharama za bima," amesema Heche.

Heche amesema matumizi ya mamilioni ya shilingi kila siku yako kwenye safari za ndani na nje za viongozi wakuu wa serikali, ambao hujilipa fedha nyingi bila kuangalia uimara wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, pamoja na mawazo ya Heche yanayokinzana na Shabiby, Pambazuko linataarifa kuwa serikali iko mbioni kuchangia bima ya afya kwa wote kupitia kodi kwenye vinywaji baridi, vileo, michezo ya kubahatisha, vipodozi na leseni kwenye vyombo vya moto.





## Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

### Rais Samia fukuza wanyanyua mabega

Na Rashid Mtagaluka

**N**I matumaini ya kila Mtanzania kwamba, mabadiliko ya mara kwa mara yanayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan yanalenga kuboresha utendaji kazi wa serikali.

Hata hivyo, bado naona juhudi za Rais Samia kubadilisha viongozi ili kupata timu inayokwenda na 'spidi' yake, zinakwama kutokana na baadhi ya wateule wake kutofahamu vyema majukumu yao.

Mabadiliko mbalimbali yaliyofanywa na Rais Samia tangu alipoapishwa kushika nafasi hiyo Machi 19, 2021, kufuatia kifo cha mtangulizi wake, John Pombe Magufuli kilichotokea Machi 17, 2021, Dar es Salaam, yanaonekana bado "hajafika."

Inavyoelekea, kundi mojawapo kati ya makundi mawili aliyorithi kutoka kwa Magufuli, ndilo linalomsumbia na litakaloendelea kumsumbia iwapo Rais Samia atachelewa kufanya uamuzi mgumu.

Kuna kundi la 'vibarua', ambao ili wafanye kazi vizuri na kwa ufanisi unaotakikana, ni lazima awepo mnyapara atakayewasimamia kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kisheria na kikanuni.

Vibarua, aghalab hufanya kazi kwa kutegea hata kama wanafahamu kazi waliyopewa ina umuhimu kiasi gani kwa jamii na taifa. Hawa wako tayari hata kuzusha visingizio ilimradi wategee.

Nakumbuka enzi za uongozi wa Rais Magufuli, hawa vibarua walikuwa wakichapa kazi kwelikweli, kwa sababu walijua msimamizi wao akipata tarifa juu ya mwenendo usiofaa katika kuwajibika, ni lazima angewang'oa haraka.

Aina ya pili ni 'madaktari,' hawa kwa kawaida huchapa kazi bila kusubiri 'mnyapara' awasimamie. Madaktari hushughulika na upasuaji wa mgonjwa bila ya kujali kiwango cha mshahara



Rais Samia Suluhu Hassan

wao wala iwapo wakimaliza kazi hiyo ya upasuaji watapewa shukrani gani!

Madaktari wa upasuaji wanachokiona fahari kubwa kwao ni mgonjwa amepona na amepona akiwa mikononi mwao basi! Hayo mengine kuhusu stahiki zao yatafuata baadaye!, hawa hawana haja ya kusimamiwa na nyapara.

Lakini, ukifuatilia kero za wananchi huku mitaani na maeneo ya vijijini, utagundua kuwa watendaji wengi wa serikali hawafanyi kazi, wao wanapoteza muda kwa kufanya shughuli zao binafsi, huku wakiwasahau wateja wao – wananchi.

Pamoja na tathmini ya Paul Makonda, aliyekuwa bosi wa idara ya uenezi ndani wa CCM, kwamba wafanyakazi wa serikali "wamererax" na hawaogopi kupokea mishahara ya bure.

Kitu kingine kinachofanya warelaksi, ni serikali kukosa mfumo mzuri wa kufuatilia na kutathmini majukumu yao kila mwezi.

Nami nimebaini kuwa vibarua ni sehemu ya wale watendaji wanaopenda 'kunyanyua mabega' huku mikono ikiwa mifukoni bila kufahamu nafasi walizonazo siyo tuzo, bali ni dhamana kuwatumikia Watanania.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546 au Barua pepe:mtagaluka@gmail.com

## Mtazamo

## Makamba na simulizi ya msamaha

Na Januari MAKAMBA

**M**WAKA 2008, nikiwa msaidizi wa Rais Jakaya Kikwete, tulikuwa ziarani wilayani Makete, wakati huo ikiwa bado ndani ya Mkoa wa Iringa, nilikuwa natumia gari na dereva wetu wa Ikulu, aliyeazimwa kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Jioni moja kuna nyaraka ilikuwa inatakiwa haraka na Rais Kikwete, hivyo nilitakiwa niifanyie kazi na nimpelekee kesho yake saa 1:00 asubuhi.

Nikamwambia dereva anifuatae saa 12:30 asubuhi ili kuwahi kuiwasilisha kwa Rais Kikwete, lakini dereva akachelewa kufika kunichukua kama tulivyokubaliana.

Nikampigia simu mara kadhaa, lakini hakupatikana na huenda simu yake ilikuwa imezimwa au imepotea.

Nikalazimika kukatafuta usafiri mwingine. Nikachelewesha nyaraka kwa Rais Kikwete na hakika akanikaripia.

Baadaye dereva akafika na akaomba nimsamehe. Akasema kuchelewa kwake kumetokana na kuitwa na 'bosi' mwingine mkubwa zaidi.

Nami nilikasirika, na nikaomba nitafutiwe dereva mwingine.

Hata hivyo, mhusika wa madereva Ikulu, akaniomba niendelee na dereva huyohuyo hadi Mbeya na huko ningepata mwingine.

Nikalazimika kuendesha na "mbaya wangu," huku akijua anaondoka kwenye nafasi yake.

Safarini wote tulikuwa kimya. Tulipokaribia Tukuyu, akaanza kutoa machozi, akisema Tukuyu ndio kwao, na ndio anarudi baada ya muda mrefu na amewaambia ndugu zake waje kumuona kwenye msafara wa Rais Kikwete.

Akaanza kuelezea historia ya maisha yake, kwamba alipomaliza darasa la saba alikuja Dar es Salaam mwaka 1984 na alipofika alianza kuuza mahindi ya kuchoma pembezoni mwa barabara, maeneo ya Mwenge.



Januari Makamba

Siku moja akaona kundi la vijana wakikimbia kutokea njia ya Lugalo; alipouliza hawa wanakwenda wapi, akaambiwa hao ni vijana wanataka kujiunga na jeshi, wanakimbia kutoka Kambi ya Jeshi Kunduchi kuelekea viwanja vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajili ya kupimwa pumzi. Palepale, akatelekeza jiko la mahindi na 'kuunga tela.'

Kwa kuwa alianzia mbio katikati, akafika wa kwanza pale viwanjani. Kule kukawa na mtu anachukua majina ya vijana waliofika kwanza. Akaandikwa na kuambiwa kesho akaripoti Kambi ya Jeshi Kunduchi kwa vipimo zaidi.

Alidamka na kesho yake asubuhi akafika geti la kambi ya jeshi, akakuta orodha inayotumika kuwaingiza watu ndani kwa vipimo zaidi. Akaingia na kazi ya kufanyiwa vipimo ikaanza. Ilipomalizika akakutwa 'yuko fiti' na hapo safari yake ya kuwa mwanajeshi ikaanza.

Jeshini huko akaingia kama mwanamichezo, mwanamieleka. Baadaye, akawa anachukuliwa na dereva mmoja kama msukuma gari kwa sababu dereva huyo alikuwa na gari kuku, ambalo halikuwa zuri sana. Ni aina ya Landrover 109.

Mwisho akajifunza gari, akawa dereva mzuri na mwenye nidhamu na ndio maana baada ya miaka kadhaa

## Tanzania yageuka pango la 'kubeti'

Na Mwandishi WETU

**B**AADA ya Serikali ya Tanzania kuvalia njuga uwepo na hata kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya, imejisahau na sasa imeruhusu janga jingine la michezo ya kamari.

Janga hilo la kamari almaarufu – kubeti, limeendelea kuwa balaa kubwa kwa ustawi wa jamii ya Watanzania, huku madhara yake yakikithiri.

Serikali hiyohiyo inayodhibiti dawa za kulevya, imeruhusu michezo ya kubeti, huku ikibainika kuwa inasukumwa na nguvu ya kodi inayokusanywa kutoka kwa wawekezaji wa michezo hiyo ya kamari.

Pambazuko imejiridhisha kuwa serikali “inapenda zaidi kodi” kutoka kwenye kamari kuliko kujali madhara yanayotokana na michezo hiyo iliyopewa jina zuri la “michezo ya kubahatisha.”

Imebainika kwamba katika kipindi cha mwaka 2019/2020, serikali hiyo ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 10.1, ikiwa ni kodi, gharama za leseni na vyanzo vingine kutoka kwenye kampuni zinazoendesha michezo ya kamari.

Pambazuko imebaini kuwa kiasi hicho ni zaidi ya asilimia 6.6 ya kiasi cha fedha kilichokusanywa na serikali ambacho kilikuwa shilingi bilioni 9.39.

Michezo hii ya kamari, ambayo awali ilikuwa kwenye kasino na majengo ya hoteli kubwa za kitalii, sasa imetapakaa kila duka “la Mangi” – kwa maana mashine za kamari ziko hata vichochoroni na vijijini.

Madhara ya michezo ya kamari ni makubwa, ikiwamo wachezaji kupata uraibu, kama ule unaowakumba watumiaji wa dawa za kulevya.

Kamari yahamia kwenye simu

Pamoja na serikali, kupitia Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (TGB), kueleza kuwa inadhhibiti michezo hiyo kwa watoto – chini ya miaka 18, hilo limeshindikana kwa kuwa sasa kamari imehamia kwenye simu.



*Dkt. Kimangale*

Vituo vya redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii, imekuwa ikitumika zaidi kutangaza na kuhimiza watu kucheza kamari, bila kueleza madhara yake.

Kukua kwa teknolojia ya intaneti, urahisi wa kupatikana kwa simu za mkononi pamoja na kutambulika kisheria kwa kamari kuwa michezo halali inayochangia pato la nchi, kumetajwa kuwa chanzo cha michezo hiyo kushamiri Tanzania.

Fursa hiyo ya teknolojia imefungua milango kwa kampuni nyingi kutoka China ‘kuvamia’ soko la michezo hiyo hapa nchini na kuisambaza hadi vichochoroni, sehemu za wazi, vituo vya mabasi na hadi vijijini.

Mbali na kusambaa kwa michezo hiyo, wataalamu wa tiba pamoja na tafiti za kisayansi zimebaini kamari ina uraibu mkubwa kuliko dawa za kulevya kama vile cocaine, heroin na nyinginezo.

Uwekezaji mkubwa unaofanywa na kampuni kutoka China, Mexico, Marekani na Afrika Kusini hapa Tanzania, kunaweza kutajwa kuwa kunachangia tatizo la afya ya akili kwa wanaocheza michezo hiyo.

Mtaalamu wa Saikolojia Tiba, Dkt.

**Habari****Tanzania yageuka pango la 'kubeti'***Inatoka Uk. 11*

Saldeen Kimangale wa Somedics Polyclinic Health Centre ya Upanga, Dar es Salaam, amezungumza na Pambazuko na kubainisha kuwa michezo ya kamari ina uraibu mkali unaosababisha matatizo ya afya ya akili kwa wanaojihusisha nayo.

Dkt. Kimangale amesema Shirika la Afya Duniani (WHO) limeorodhesha mchezo wa kamari kuwa mojawapo ya chanzo cha magonjwa ya afya ya akili kwa binadamu.

Amesema kwa mujibu wa kitabu cha mwongozo wa utambuzi wa magonjwa ya akili ukurasa wa 358 chini ya kichwa cha habari 'Gambling Disorder,' kamari inaweza kusababisha ugonjwa wa kucheza kamari (uraibu).

Amesema kamari inaweza kusababisha uraibu kwa ile shauku ya kupata zaidi na kwa sababu hiyo anayejihusisha nayo anasikia raha ya kupata zaidi, na pale anapoteza anahisi maumivu makali.

Dkt. Kimangale amesema kuwa mwenye uraibu wa kamari anapokuwa amepoteza fedha, hupenda kulipa kisasi kwa kuweka fedha zaidi na kwamba tabia hiyo ikidumu kwa muda mrefu, muhusika hupata huzuni, hasira, kukosa utulivu, kukosa umakini kwenye kazi, kukosa usingizi na hamu ya kula.

"Wagonjwa wa aina hiyo tumekuwa tukiwatibu kwa tiba inayohusiana na mabadiliko ya tabia na hatua za mabadiliko ikiwa ni pamoja na kumuwezesha mgonjwa kujenga utayari wa kubadili tabia na wale wanaoweza kushiriki matibabu vizuri wanapona kabisa," amesema Dkt. Kimangale na kuongeza

Kuhusu takwimu za uraibu wa kamari nchini, Dkt. Kimangale amesema ingawa Tanzania haijatoa takwimu rasmi za wenye changamoto ya afya ya akili itokanayo na uraibu wa kamari, uzoefu wa kimazingira unaonesha tatizo ni kubwa kwa sababu wanaocheza ni wengi na vyombo vinavyoendesha michezo hii pia ni vingi na vimesambaa hadi kwenye

**Kamari**

vitongoji.

Changamoto ya afya ya akili pia imechomoza katika ripoti ya Mkagazi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere kwa mwaka 2022/2023 aliyotoa hivi karibuni.

CAG Kichere amesema kuna idadi kubwa ya watu wenye tatizo la afya ya akili na kutokana na kutokuwapo fungu la fedha pamoja na ukosefu wa wataalam wa ustawi wa jamii katika ngazi za vijiji na mitaa.

Ingawa ripoti hiyo ya CAG haikugusia chanzo cha changamoto hiyo ya afya ya akili, lakini imeweka wazi kuwa, ukosefu mkubwa wa huduma za kisaikolojia katika ngazi ya jamii kwa watu wenye mahitaji maalum haujajumuishwa katika mipango na sera ya afya za serikali.

"Vituo vingi havipati huduma za utengamo kwa ajili ya kusaidia wagonjwa kupona, ambapo kati ya mikoa 28, ni mikoa mitano pekee ndiyo ina vituo vya utengamo vya huduma za afya ya akili," amesema CAG Kichere.

Mhadhiri Msaidizi Kitengo cha Saikolojia cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Magolanga Shagembe, anaunganisha uraibu wa kamari au 'kubeti' kama ulivyo wa pombe, sigara na dawa za kulevya na au ulevi mwingine wowote.

Amesema mtu aliyefika kwenye ulevi huo hawezi kukaa bila kubeti, na asipobeti anajisikia vibaya kwenye akili, mwili na hisia zake; hivyo anabeti ili kuondoa maumivu anayokuwa nayo.

Anashauri watu waliofikia kwenye

## Tanzania yageuka pango la ‘kubeti’

*Inatoka Uk. 12*

hatua hiyo ya uraibu wasihukumiwe, wasaidiwe kwa kuwapatia msaada wa tiba ya afya ya akili, ili warudi kwenye majukumu yao ya kila siku.

Madhara makubwa ya uraibu wa michezo ya kamari mbali na kupata afya ya akili ya moja kwa moja – ikiwamo ukichaa, ni pamoja na kuzidisha umasikini, kudhoofu kwa afya ya mwili na hata kujiua.

Katika ripoti ya utafiti ya Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Auckland, New Zealand iliyopewa jina la The epidemiology and Impact of gambling – harm ya Juni 2017, yaani magonjwa ya mlipuko na madhara yatokanayo na kamari, imesema kuna ongezeko kubwa la michezo ya kamari inayofanyika kibiashara na inatarajiwa kuongezeka zaidi bila kujali madhara yanayoweza kuwakabili wanaoshiriki katika michezo hiyo.

Ripoti hiyo iliyolenga kuangalia madhara yatokanayo na kamari iliwasilishwa kwenye mkutano maalumu wa WHO Juni 2017 uliangazia vile, dawa za kulevywa na tabia hatarishi, ikiwamo uraibu wa kamari.

Katika ripoti hiyo, watu waliokuwa wakikabiliwa na matatizo ya afya ya akili duniani kutokana na ushiriki wa kamari wamekuwa wakiongezeka mara tatu zaidi kila mwaka.

Hata hivyo, ripoti hiyo haisemi dunia nzima ina wagonjwa wangapi wanaotokana na michezo ya kubeti.

Ripoti hiyo iliyotayarishwa na Profesa Abbott wa chuo hicho, ilieleza kuwa mwaka mmoja kabla, kesi za msongo wa mawazo na uraibu utokanao na ushiriki wa michezo ya kamari ziliripotiwa kuongezeka kutoka asilimia moja hadi asilimia sita.

Utafiti mwingine ulifanywa Juni 2021 na Aprili 2022 na kuchapishwa kwenye Jarida la Kimataifa la Afya ya Jamii (IJPH), Mei 19, 2023 na kupewa jina la uchambuzi wa vijana wacheza kamari na unyanyasaji wa wenza jijini Mwanza –

unaonyesha madhara makubwa ya uraibu wa kamari.

Utafiti huo ulishirikisha wataalamu kutoka taasisi sita za kimataifa kutoka Ujerumani na Tanzania kupitia Mwanza Intervention Trials Unit pamoja na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) Kituo cha Mwanza.

Utafiti huo umeainisha namna tabia ya uchezaji kamari na uraibu utokanao na kamari unavyochochea unyanyasaji na kuathiri familia, ambapo imebainika kuwa waathirika zaidi ni watu walio katika umri wa miaka 22- 42 ambao ni vijana.

Wataalam hao walieleza kuwa uwiano wa unyanyasaji wa wenza unaotokana na ushiriki kweye michezo ya kamari unaonesha upo katika kiwango cha juu nchini Tanzania ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.

“Wanaume ndio washiriki wakubwa wa michezo ya kamari, huku ikihusishwa na ukatili wa kudhuru mwili, ukatili wa kingono, hisia na ukatili wa kiuchumi kutokana na madhara ya kiakili wanayoyapata washiriki wa michezo hiyo.” imesema sehemu ya ripoti hiyo.

## Makamba na simulizi

*Inatoka Uk. 10*

akaazimwa Ikulu.

Wakati ananieleza hiki kisa, machozi yanamtoka. Nikamsamehe.

Wiki iliyopita, nikamuomba bado yumo kwenye msafara wa Ikulu. Bado ana nidhamu. Nikamuomba nielezee kisa hiki kwa umma. Akakubali.

Hakika maisha yake ni elimu ya kutokata tamaa na kuenda kile unachopenda na kufanya kwa heshima, na unyenyekevu mkubwa.

**Tusameheane.**

•Mwandishi wa makala haya ana Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

## Kenya

## Ruto abadili gia, upinzani wamkubali

Na Julius MKAMBI,  
Nairobi

**R**AIS wa Kenya, Dkt. William Ruto, kama ilivyokuwa mtangulizi wake, Uhuru Kenyatta, alipata wakati mgumu kujipenyeze kwenye ngome za kisiasa za mpinzani wake mkuu, Raila Odinga.

Licha ya kuteua baadhi ya watu kutoka ngome ya kisiasa ambazo Raila anaungwa mkono kuwa mawaziri na kuwapa nyadhifa zingine ndani ya serikali, bado alijikuta akipata wakati mgumu kukubalika na wananchi wengi "wanaopenda" Raila.

Haikushangaza kumsikia Naibu Rais Rigathi Gachagua akifananiha serikali na kampuni akisisitiza watakaopewa umuhimu kuteuliwa na Rais Ruto ni 'wenye hisa,' akimaanisha watu wale kutoka kwa ngome ambazo walimpigia kura kwa wingi Rais Ruto katika uchaguzi mkuu uliyopita.

Mbinu aliyotumia Rais (mstaafu) Kenyatta kukubalika kwenye ngome za upinzani ni 'handshake' aliyofanya na Raila mwaka 2018 ambayo ilipunguza joto la kisiasa hususan baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2017 ambapo matokeo yake yalifutwa na mahakama, na kwenye marudio ya uchaguzi huo, upinzani ukiongozwa na Raila uliususia, wakisisitiza Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) haukutekeleza yale ambayo waliagizwa na mahakama.

Raila amekua mwiba mgumu kwa kila anayechaguliwa kuwa Rais wa Kenya kuanzia kwa Mwai Kibaki, Kenyatta na sasa Ruto.

Itakumbukwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2022 ulioshuhudia makamishna wa IEBC wakitofautiana, ambapo baadhi ya walipinga matokeo ya mwisho yaliyotangazwa na aliyekuwa mwenyekiti wao, Wafula Chebukati ya kumtangaza Ruto mshindi wa kiti cha urais.

Ruto ambaye kisiasa aliibuliwa na



Kenya, Dkt. William Ruto

rais wa awamu ya pili, Daniel arap Moi na kujikuta akikomazwa na Raila wakati wawili hao walipokuwa kwenye chama kimoja cha Orange Democratic Movement (ODM).

Hata hivyo, katika mazingira ya sasa, Ruto anaonekana amefanikiwa kujipenyeze kwenye ngome ya mpinzani wake mkuu.

Hii ni baada ya Rais Ruto kuweka wazi kwamba ataongoza kampeni ya kuhakikisha Raila anachaguliwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), akimrithi aliyekuwa Waziri Mkuu wa Chad, Moussa Faki, wakati uchaguzi utakapofanyika.

Rais Ruto amesisitiza kumuunga mkono Raila ni kuweka mbele maslahi ya taifa na kwamba mpinzani wake huo kisiasa ametosha kuvaa viatu vya Faki.

Kitendo hiki kilichooneshwa na Rais Ruto kimebadili uepeo wa kisiasa, ingawa bado wapo baadhi ya wanasiasa wanaohisi hii ndiyo njia pekee ya kiongozi huyo wa nchi - siyo tu kujivunia kuanza kuungwa mkono kwenye ngome za mpinzani wake mkuu, mbali pia 'kumuondoa' Raila katika siasa za Kenya.

Moja ya masharti kwa kiongozi yoyote anayechaguliwa Mwenyekiti wa AU ni kujitenga na siasa za nchi husika hii ni kumaanisha endapo Raila atamrithi Faki, basi atalazimika kutojihusisha na siasa za Kenya kwa miaka miwili.



# *Tangaza na* **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au

Barua- Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

## Ana kwa Ana

### Sabi: Nchi isiyothamini wasanii wake, ni mfu

**S**ABI John Kitaule, ni jina linalokua na kuendelea kubeba sifa katika medani za sanaa ya uchoraji. Ni binti wa Kitanzania ambaye ameamua maisha yake yasimama kwenye sanaa. Ana maono kwamba Tanzania inaweza kupata sifa zaidi kupitia sanaa, huku akibainisha kuwa nchi isiyothamini wasanii wake, haina mwelekeo. Katika mahojiano haya ya Ana kwa Ana na mwandishi wa Pambazuko, anaeleza mengi kuhusu sanaa hiyo ya uchoraji.

**Swali:** Je, lini ulianza kupenda sanaa ya uchoraji?

**Jibu:** Nilianza kupenda kuchora nikiwa na umri mdogo. Tangu nina miaka mitatu, na huenda chini ya hapo – nilikuwa nachora kwenye kuta ndani ya nyumba na kila mahali.

Nilikuwa nasimuliwa na wazazi wangu kwamba nilikuwa mtoto wa kuchorachora vitu visivyoeleweka, ingawa walikuwa wakinisifu.

Nilipokuwa najitambua, wazazi walinipeleka kwenye darasa la uchoraji, baada tu ya kuwa nimeanza elimu ya msingi.


Hata hivyo, niliweka maanani zaidi kwenye sanaa ya uchoraji baada ya kuwa shule ya sekondari ambapo nilipata mwalimu mzuri zaidi wa sanaa hiyo ya uchoraji na hapo nikaamua kuwa hiyo ndiyo itakuwa kazi yangu.

**Swali:** Je, ni kipaji cha kuzaliwa nacho au umejifunza ukubwani?

**Jibu:** Nilizaliwa nacho kwanza, halafu nikakiendeleza kama ambavyo nimeeleza hapo awali.

**Swali:** Je, sanaa ya uchoraji ina mchango gani katika maisha yako na labda familia yako?

**Jibu:** Mimi nachukulia sanaa hii ya uchoraji kuwa kazi yangu, na ninaheshimu sana, pia nimebahatika kwa sababu familia yangu inaheshimu kwamba nimechagua kufanya kazi hii



*Sabi John Kitaule*

na wananisukuma na kunisaidia kufanya vizuri zaidi.

Na pia sanaa ya uchoraji inanilipa fedha kidogo, ingawa kwa sasa sijaifanya kuwa biashara zaidi, kwani nataka nitambulike na kuaminika zaidi kwanza.

Hivi sasa nafanya sanaa hii ya uchoraji kwa sababu napenda sanaa ya kuchora na ninaweza kuelezea habari na hadithi nyingi kupitia michoro yangu.

**Swali:** Changamoto zipi unakumbana nazo katika kufanya kazi zako za sanaa?

**Jibu:** Watu wengi – hasa hapa Tanzania, wanaona wasanii siyo muhimu sana na hawapewi stahiki na heshima inayostahili.

Pia kazi za sanaa hapa Tanzania hazilipi, watu wanatuchukulia poa sana sisi wasanii wa uchoraji, au niseme wasanii kwa ujumla.

Wapo baadhi ya watu hawaoni umuhimu wa sanaa, ndiyo maana wasanii wa uchoraji hawathamini sana.



## Ana kwa Ana

### Sabi: Nchi isiyothamini wasanii wake, ni mfu

Inatoka Uk. 16

**Swali:** Msanii gani wa uchoraji unayemhusudu, Tanzania na hata nje?

**Jibu:** Hapa Tanzania nampenda sana Tinga Tinga (Edward Tinga Tinga), ambaye ni msanii wa uchoraji na uchongaji.

Pia, nampenda sana Salvador Dali, huyu ni ni mchoraji kutoka Hispania. Huyu ni msanii anayeheshimika duniani kote na amekuwa mhimili wangu katika kujifunza zaidi.

Zipo kazi nyingi zinavutia na kunipa hamasa ya kufanya vyema zaidi. Hakika nafurahi kuona ukuu na umaarufu wake, nami naahidi kufika huko.

Upo pia, Cheri Samba ambaye ni mchoraji kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huyu napenda kazi zake kwa sababu haogopi kutumia rangi mbalimbali na alama za kazi zake ni nzurii.


**Swali:** Una ujumbe gani kwa wale wanaopenda sanaa ya uchoraji, lakini hawana fursa ya kuonesha ubunifu wao kwenye fursa kubwa?

**Jibu:** Napenda kuwaasa watu wanaopenda sanaa ya uchoraji kuanza ama kuendelea endapo walisimama kwa muda kutokana na sababu mbalimbali. Kazi za sanaa hazina umri, muda wowote unaweza kuanza na kufanikiwa.

Fursa zipo tena kwa sasa ulimwengu wa sanaa za uchoraji una kuwa kasi, hivyo wenye kipaji au matamaniao ya kuchora, wachore sana. Pia wajifunze kutoka kwa wengine wenye uzoefu na kuwa wabunifu zaidi.

**Swali:** Maonesho gani makubwa ambayo umewahi kushiriki? Iwe ndani au nje ya Tanzania?

**Jibu:** Nilianza na 'Group Shows 2020' iliyofanyika Nafasi Arts Space, 2021 hapa Dar es Salaam na baadaye nikafanya onyesho la binafsi la kwanza ambalo nililipa jina la "The Quite Mind Art Exhibition," 2022 na kuendelea na maonesho mengine pale Range Gallery



na pia Nafasi Arts Space .

Mwaka 2023 nilishirikishwa kule Afrika Kusini ambapo nilifanya maoesho kadhaa nikiwa na wasanii wengine wa uchoraji.

Mwaka 2024 nimeanza na maonesho binafsi (ya mtu mmoja) – yakiwa ni ya pili ambayo nimeyapa jina la "Emerged From Slumber wa Too Early" ambayo yanaendelea kuwepo hapo Nafasi Arts Space, Mikochei, Dar es Salaam. Haya maonesho yalianza Machi 8 na yataisha Aprili 8, 2024.

**Swali:** Nini ndoto yako katika safari yako ya sanaa ya uchoraji?

**Jibu:** Ndoto yangu kubwa ni kufungua sehemu kubwa ya maonesho ya sanaa ambapo watu watapata fursa ya kuendeleza vipaji vyao na pia kuwapa mwanga watu wengine kuelewa maana halisi ya sanaa ndani ya jamii.

Imani yangu ni kwamba kupitia sehemu hiyo, thamani ya wasanii itapanda na kuonekana zaidi kwa jamii ya Watanania na watu wengine.

Ileweke kuwa sisi wasanii ni kioo cha jamii na ndiyo maana kwenye nchi nyingine, wasanii wanaheshimika na kupewa thamani kubwa zaidi.

## Kabumbu

### Yanga, Simba wameweka heshima

Na Mwandishi WETU

**A**CHANA na matokeo ya mechi za Mamelodi Sundowns dhidi ya Yanga pale Pretoria, Afrika Kusini na ile ya Al Ahly dhidi ya Simba katika dimba la Cairo International ndani ya Jiji la Cairo, Misri.

Kitu kimoja kinachojitokeza kwa wapenda soka wengi Afrika na pengine maeneo mengi duniani, ni heshima ambayo timu hizo za Tanzania zimeweka mwaka huu kwenye mashindano ya vilabu barani Afrika.

Tanzania imeingia katika historia ya kuwa nchi pekee ya Afrika kuingiza timu mbili katika hatua ya robo fainali ya Klabu Bingwa Barani Afrika mwaka huu. Hakuna nchi nyingine iliyoweza kufanya hivyo.

Lakini, siyo tu kuingiza timu mbili, kiwango cha mpira ambacho kimeonyeshwa na klabu ya Yanga ilipotelewa kwa njia ya matuta na Mamelodi, kimewaacha watu wengi vinywa wazi kwani hawakuamini kile walichokiona.

Droo ya mechi hizo ilipopangwa na Yanga kupangiwa Mamelodi, watu wengi, wakiwamo wachambuzi wa soka nchini, waliipa Mamelodi nafasi kubwa ya kufuzu hatua ya nusu fainali kirahisi kwa



*Mchezaji wa Yanga ya Tanzania, Dickson Job (wenye jesi ya kijani), akiwahenyeshwa wapinzani wake wa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini katika mcheso uliofanyika Pretoria, Afrika Kusini. Yanga ilifungwa 3-2 kwa njia ya mikwaju ya penati. (Picha kutoka CAF).*

maelezo kuwa timu hiyo ilikuwa kwenye kiwango bora na kikubwa kulinganisha na Yanga.

Wengi hawakuipa Yanga nafasi licha ya mwaka jana kuonyesha maajabu na kufanikiwa kufikia hatua ya fainali ya Kombe la Washindi Afrika na kulikosa kombe hilo kwa kanuni za goli la ugenini.

Wengi waliamini kuwa itakuwa mechi rahisi kwa Mamelodi ambayo ni bingwa wa Afrika Football League (AFL) iliyoanzishwa mwaka jana na kushirikisha Simba miongoni mwa timu nyingine nane Afrika.

Wengi waliamini kuwa kiwango cha Mamelodi ni kikubwa sana kwa timu kama Yanga ambayo hajacheza hatua ya makundi ya Klabu Bingwa Afrika kwa takribani miaka 25.

Hivyo, wakafikia uamuzi kuwa Mamelodi wataiotoa Yanga kirahisi katika hatua hiyo.

Ni kweli Mamelodi wameitoa Yanga, lakini kile kilichoonekana katika mechi mbili baina ya timu hizo kimewaacha watu wengi vinywa wazi kutokana na kiwango kikubwa ambacho Yanga wamekionyesha.

Baada ya kukamilika kwa mechi ya kwanza katika uwanja wa Benjamin

Mkapa, Dar es Salaam kwa suluhu, wengi wakaamini kuwa Yanga itakapofika Afrika Kusini kwa ajili ya mechi wa marudiano, basi “watakiona cha moto.”

Wengi wakatoa rekodi kuwa Mamelodi hajawahi kufungwa nchini kwake katika kipindi cha misimu mitatu iliyopita, hivyo haitakuwa rahisi kufugwa na Yanga.

Lakini, licha ya

*Endelea Uk. 19*

## Yanga, Simba wameweka heshima

*Inatoka Uk. 18*

utabiri huo, Aziz Ki alifumua shuti lililogonga mwamba na mpira, kwa macho ya mtazamaji wa kawaida, kuonekana ukitua ndani ya mstari wa goli la Mamelodi.

Mwamuzi akasimamisha pambano ili waamuzi wasaidizi wanaotumia marudio ya picha video na teknolojia nyingine kuliangalia kwa undani goli lile.

Wakati hayo yakitokea kukawa na picha za marudio katika televisheni, tena kwa mwendo wa polepole na watu wengi, wakiwamo watangazaji wazoefu wa vituo mbalimbali vya luninga waliokuwa wakitangaza mechi hiyo moja kwa moja, wakajiridhisha kuwa mpira ule ulikuwa umetua ndani ya goli la Mamelodi hivyo wakawa wanasubiri tu mwamuzi aziite timu katikati ili kuanza mchazo upya baada ya goli hilo.

Kwa maajabu ya wengi, mwamuzi aliyesaidiwa na waamuzi wasaizidi wa video, akasema kuwa mpita huo haukuvuka mstari, hivyo siyo goli.

Kwa bahati mbaya teknolojia ya 'goal-line' haikutumuika na kama ilitumika picha zake hazikuonyesha kwa watazamaji ili nao waridhike na uamuzi.

Matokeo yake, mpaka wakati huu watu wengi, wakiwamo baadhi ya mashabiki wa Mamelodi wanaamini kuwa Yanga ilikuwa imepokwa lile goli ambalo kama lingekubaliwa, lingekuwa limeingiza timu hiyo katika hatua ya nusu fainali.

Kocha wa Mamelodi mwenyewe anakiri kuwa hata kama yeye angekuwa Yanga, basi angeamini kuwa lile lilikuwa goli halali.

Lakini, ukiacha utata wa goli hilo, hatua ya Yanga kuizua Mamelodi isiweze kufunga goli katika mechi hizo mbili, nayo imeacha gumzo kubwa watu wengi wakishangazwa na kiwango kilichoonyesha na Yanga mbele ya miamba hiyo ya soka barani Afrika.

Wengi waliisifia Memelodi kama timu mahiri ambayo ikicheza inamfunga mpinzani wake vile itakavyo. Wakadai

kuwa salama ya Yanga katika mechi dhidi ya timu hiyo itatokana na uwezo wake wa kuzuia wasifungwe.

Kilichotokea ni kuwa katika mechi hizo mbili Memelod wameshindwa kutimiza kile ambacho wachambuzi wengi waliamini kuwa wangekifanya dhidi ya Yanga - kuifunga.

Lakini kwa upande wa pili, Yanga imefanikiwa kufanya kile ambacho wachambuzi wengi waliamini kuwa haiwezi kukifanya mbele ya Mamelodi, kuizua timu hiyo mahiri isipate goli dhidi yake.

Kwa maana nyingine, kati ya timu hizo mbili ni Yanga ambayo imefanikiwa kutimiza malengo ambayo yaliwekwa na wachambuzi wa soka nchini na kwingineko.

Kwa maana hiyo, mtu hatakosea iwapo atasema kuwa katika mechi hizi mbili Yanga ilikuwua bora zaidi ya Mamelodi kwa sababu Yanga ilifanikiwa kutekeleza kile ambacho wachambuzi wengi waliamini kuwa haiwezi.

Simba nao, ingawa wametolewa katika hatua hiyo, lakini 'usumbufu' waliouyeshesha kwa Al Ahly, hasa ikizingatiwa kuwa mwaka huu Simba haiko katika kiwango cha juu cha ubora, imeonyesha kuwa ni timu kubwa na imara.

Ukiangalia takwimu za mechi mbili kati ya timu hizo, ni Simba ambayo inaonekana kuwa na takwimu nzuri za umiliki wa mchezo na mashambulizi, lakini hawakuwa na 'ukatili tu' wa kuweka mpira wavuni.

Kwa ujumla mafanikio ya Yanga na Simba mwaka huu katika mashindano ya soka Afrika, yameacha gumzo kubwa kuhusu viwango vya timu za Tanzania.

Ni wakati sasa viongozi wa timu hizo na nyingine ambazo zitapata fursa ya kushiriki mashindano ya Afrika mwakani, kufanya maandalizi mazuri ili watakaposhiriki mwakani waonyeshe ushindani mkubwa kama walivyofanya Simba na Yanga mwaka huu.

# Tausi mweupe...



*Viembe hawa wazuri sana ni spishi adimu ya tausi. Tausi weupe siyo albino; wana mabadiliko ya kijeni ambayo yanajulikana kama Leucism, ambayo husababisha ukosefu wa rangi kwenye manyoya. Tausi wa aina hii hupatikana zaidi maeneo machache nchini India na Austraria. (Picha na mtandao).*

**GAZETI** hili lilianzishwa 2021, kuandalwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

